# SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 27 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) MEI 2023

# SERIKALI YAAJIRI WATUMISHI 21,200 KADA YA UALIMU, AFYA



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Angellah Jasmine Kairuki akitangaza ajira za Watumishi wa Kada ya Ualimu na Afya katika mkutano wake na waandishi wa habari uliofanyika tarehe 12 Aprili, 2023 jijini Dodoma.*

**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz** **Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

## AJIRA ZA SERIKALI NI BURE, TUEPUKE RUSHWA NA MATAPELI

Hivi karibuni Serikali imetangaza ajira za Watumishi wa Kada za Ualimu 13,130 wa Shule za Msingi na Sekondari watakaofanya kazi chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Afya 8,070 kwa ajili ya Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya na Zahanati.

Tangazo hilo lilitolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Angellah Jasmine Kairuki katika mkutano wake na waandishi wa habari uliofanyika tarehe 12 Aprili, 2023 jijini Dodoma.

Waziri Kairuki alisisitiza kuwa ajira hizo zinatolewa bure ambapo waombaji walitakiwa kutuma maombi kwa njia ya mtandao kupitia kiunganishi cha ajira.tamisemi.go.tz. Muda uliowekwa kwa ajili ya kutuma maombi ya ajira hizo ulimalizika Aprili 25, 2023 na taratibu nyingine zinaendelea ili kukamilisha ajira hizo.

Upo uwezekano kuwa wapo matapeli wanaoweza kujitokeza kudanganya wanachi ili watoe fedha kwa kisingizio cha kuwapatia ajira jambo ambalo ni kinyume cha sheria. Ni muhimu kukumbushana kuwa Serikali inaendesha zoezi hili kwa haki na kuzingatia sifa na vigezo vilivyoainishwa na hakuna malipo yoyote yanayohitajika katika zoezi hilo.

Hivyo, tuepuke matapeli au kushawishika kutoa rushwa kwa mtu yeyote na pale vinapojitokeza vitendo vya namna hiyo tusiache kutoa taarifa kwenye vyombo vinavyohusika ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa kwa haraka.

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Paulina M. Nkwama

**Wajumbe**
Richard L. Odongo
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

**Mhariri Mkuu**
Gerard J. Chami

**Mhariri**
Adili J. Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas G. Ogunde

## KATUNI



# SERIKALI YAAJIRI WATUMISHI 21,200 KADA YA UALIMU, AFYA

**Na Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Serikali imetangaza ajira za Watumishi wa Kada za Afya 8,070 kwa ajili ya Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya na Zahanati pamoja na Ualimu 13,130 wa Shule za Msingi na Sekondari watakaofanya kazi chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Tangazo hilo lilitolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Angellah Jasmine Kairuki katika mkutano wake na waandishi wa habari uliofanyika tarehe 12 Aprili, 2023 jijini Dodoma ambapo alisistiza kuwa waombaji wa ajira hizo wanatakiwa kutuma maombi kwa njia ya mtandao kupitia kiunganishi cha *ajira. tamisemi.go.tz.*

"Wahitimu kutoka kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu, Vyuo vya Ualimu na Vyuo vya Afya vinavyotambuliwa na Serikali wanatangaziwa kutuma maombi ya kazi kuanzia tarehe 12 - 25 Aprili, 2023. Nafasi za ajira zilizopo ni kwa wahitimu wa Astashahada (*Certificate*), Stashahada (*Diploma*) na Shahada (*Degree*)," alisema Kairuki.

Akizungumzia kuhusu ajira za walimu Waziri Kairuki alisema kuwa tangazo hilo linawahusu wahitimu wa Kozi za Ualimu kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2022 huku akiongeza kuwa waombaji waliowahi kutuma maombi yao awali kupitia mfumo wa maombi ya ajira watahitajika kuhuisha taaarifa zao kwenye




*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Angellah Jasmine Kairuki akitangaza ajira za Watumishi wa Kada ya Ualimu na Afya katika mkutano wake na waandishi wa habari uliofanyika tarehe 12 Aprili, 2023 jijini Dodoma.*

# SERIKALI YAAJIRI WATUMISHI 21,200 KADA YA UALIMU, AFYA



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akiwa katika Mkutano wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Angellah Jasmine Kairuki (hayupo pichani) na waandishi wa wahabri uliofanyika tarehe 12 Aprili, 2023 jijini Dodoma.*

mfumo huo.

Alieleza kuwa nafasi za ualimu wa shule za msingi ninazohitajika kuombwa ni Mwalimu Daraja la III A mwenye Astashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi, Elimu ya Michezo, Elimu Maalum na Elimu ya Awali (*certificate in primary education*); Mwalimu Daraja la IIIB awe na stashahada ya ualimu (diploma) waliosomea elimu ya Msingi; pamoja na Mwalimu Daraja la IIIC inayohitaji mwombaji mwenye shahada ya Ualimu kwa Elimu ya Awali.

"Nafasi za ualimu wa shule za Sekondari ni Mwalimu Daraja la III B inayohitaji mwaombaji awe mwenye Stashahada (*Diploma*) ya Ualimu aliyesomea Elimu Maalum kwa masomo ya *English Language, Literature in English, Biology, Chemistry, Physics na Mathematics*; Mwalimu Daraja la III C awe mwenye Shahada ya Ualimu aliyesomea Elimu Maalum kwa masomo ya *English Language, Literature in English, Biology, Chemistry, Physics na Mathematics* pamoja na Mwalimu Daraja la III B mwenye Stashahada ya Ualimu wa somo la *English Language, Literature in English, Biology, Chemistry, Physics na Basic Mathematics*," alisema Waziri Kairuki.

Aliendelea kueleza nafasi zingine za walimu watakaoajiriwa kwa upande wa shule za sekondari kuwa ni Mwalimu Daraja la III C ambapo mwombaji anatakiwa kuwa na Shahada ya Ualimu wa somo la *English Language, Literature in English,*



*Washiriki waliohudhuria Mkutano wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Angellah Jasmine Kairuki na Waandishi wa habari uliofanyika tarehe 12 Aprili, 2023 jijini Dodoma kwa lengo la kutangaza ajira za watumishi wa Umma kaika kada ya Ualimu na Afya.*

# SERIKALI YAAJIRI WATUMISHI 21,200 KADA YA UALIMU, AFYA

*Biology, Chemistry, Physics na Basic* Mathematics *pamoja na* Fundi Sanifu wa Maabara ambaye inapaswa kuwa na Stashahada ya Ufundi Sanifu Maabara au Stashahada ya Sayansi na Teknolojia ya Maabara.

Akielezea sifa za jumla, Waziri Kairuki alisema mwombaji lazima awe raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45; awe na vyeti kamili vya mafunzo ya fani aliyosomea (Cheti cha Kidato cha Nne, Sita, Taaluma na usajili kamili (Full Registration) au Leseni hai ya kufanya kazi ya taaluma husika); asiwe Mwajiriwa wa Serikali au Mwajiriwa wa Hospitali za Mashirika ya Dini ambaye mshahara wake unalipwa na Serikali; awe hajawahi kufukuzwa, kuacha kazi au kustaafishwa katika Utumishi wa Umma; awe na Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA); na aambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.

Waombaji walioajiriwa kwa mkataba wa ajira kutoka kwa Wadau wa Maendeleo katika Sekta ya Afya wanatakiwa kuambatisha nakala za mkataba na barua za uthibitisho kutoka kwa Wakurugenzi wa Halmashauri husika. Pia, waombaji wenye Ulemavu na sifa zilizoainishwa watume maombi yao pia kupitia mfumo. Aidha, maombi yao yaeleze aina ya ulemavu alionao na kuambatisha picha na uthibitisho wa daktari kutoka katika hospitali za Serikali," Waziri alisisitiza.

Pamoja na hayo, Waziri alielekeza kuwa waombaji wote wawe tayari kufanya kazi katika Halmashauri/Vituo watakavyopangiwa; wawe tayari kufanya kazi na Mashirika au Taasisi zilizoingia Ubia na Serikali; baada ya kupangiwa kituo cha kazi, hakutakuwa na nafasi ya kubadilishiwa kituo cha kazi; waombaji wote wahakikishe wanajaza taarifa zao na kuambatisha nyaraka zote muhimu kwenye mfumo.

Dirisha la kupokea maombi hayo lilifungwa tarehe 25 Aprili, 2023 saa 05:59 usiku ambapo taratibu nyingine za ukamilishaji wa ajira hizo zinaendelea.






*Washiriki waliohudhuria Mkutano wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Angellah Jasmine Kairuki na Waandishi wa habari uliofanyika tarehe 12 Aprili, 2023 jijini Dodoma kwa lengo la kutangaza ajira za watumishi wa Umma kaika kada ya Ualimu na Afya.*

OFISI YA RAIS
**TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)**

# Asante



**MHE. DKT SAMIA SULUHU HASSAN**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Tunakushukuru sana na kukupongeza kwa jitihada kubwa za kuboresha na kuimarisha Sekta ya Elimu nchini hata kuridhia na kutoa kibali cha kuajiri Walimu 13,130 wa Shule za Msingi na Sekondari nchini.

Aprili 12, 2023.

ume Utumishi wa Walimu Tanzania    www.tsc.go.tz

# WAZIRI KAIRUKI AWASILISHA BAJETI YA SHILINGI TRILIONI 9 KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

- *Shilingi 9,144,021,699,000 zaombwa kidhinishwa kwa matumizi ya kawaida, mishahara, mikoa, halmashauri, TSC na miradi ya maendeleo;*
- *Wanafunzi 2,411 wenye mahitaji maalum waandikishwa ikiwa ni wasichana 1,211 na wavulana 1,200;*
- *Ongezeko la wanafunzi 88,417 walioandikishwa mwaka 2023 sawa na asilimia 3.38 ikilinganishwa na mwaka 2022, limetokana na Uhamasishaji wa Jamii, Ujenzi wa Vituo Shikizi na kuendelea kutoa Elimu Msingi bila ada;*
- *Mahitaji ya Walimu katika Shule za Msingi yabainika kuwa 362,189 kwa kutumia uwiano wa Mwalimu mmoja kwa Wanafunzi 45 kwani Walimu waliopo ni 175,864 na upungufu ni 186,325 sawa na asimilia 51.44;*
- *Mahitaji ya Walimu kwa Shule za Sekondari yabainika ni 174,632 ikilinganishwa na waliopo 84,700 inayoleta upungufu wa Walimu 89,932 sawa na asilimia 51.5.*

**Na Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (Mb), amewasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 siku ya Ijumaa Aprili 14, 2023 Bungeni Jijini Dodoma.

Waziri Kairuki aliomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 9,144,021,699,000 (zaidi ya Trilioni Tisa) ambazo ni Matumizi ya Kawaida ya Ofisi, Mishahara ya Watumishi, Mikoa, Halmashauri,



Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na Miradi ya Maendeleo.

Waziri Kairuki alitoa maelezo ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023 kuwa katika eneo la Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu Msingi jumla ya wanafunzi wa Elimu ya Awali walioandikishwa walikuwa 1,411,810 sawa na asilimia 103.52 ya lengo la kuandikisha wanafunzi 1,363,834 ukilinganisha na mwaka 2023 ambapo wanafunzi 1,500,227 wameandikishwa ikiwa ni asilimia 109.37 ya lengo la kuandikisha wanafunzi 1,371,690 wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalum 2,411 ikiwa 1,211 ni wasichana na wavulana 1,200.

Waziri Kairuki alisema mafanikio ya kuandikisha Wanafunzi wengi kwa ongezeko la wanafunzi 88,417 sawa na

# WAZIRI KAIRUKI AWASILISHA BAJETI YA SHILINGI TRILIONI 9 KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

asilimia 3.38 ikilinganishwa na Wanafunzi walioandikishwa mwaka wa 2022 yametokana na Uhamasishaji wa Jamii, Ujenzi wa Vituo Shikizi na kuendelea kutoa Elimu Msingi bila ada.

Kuhusu upungufu wa Walimu, Waziri Kairuki alisema hadi kufikia mwezi Februari, 2023 mahitaji ya Walimu katika Shule za Msingi yalikuwa 362,189 kwa kutumia uwiano wa Mwalimu mmoja kwa Wanafunzi 45 ambapo Walimu waliopo ni 175,864 na upungufu ni 186,325 sawa na asimilia 51.44 ya mahitaji.

Aidha, alisema mahitaji ya Walimu kwa Shule za Sekondari ni 174,632 ambapo waliopo ni 84,700 na upungufu ni walimu 89,932 sawa na asilimia 51.5 lakini pia mahitaji ya Walimu kwa Shule za Sekondari yanatokana na masomo yanayofundishwa.

Kuhusu utekelezaji wa Afya ya Msingi Waziri Kairuki alisema, katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 ziliidhinishwa Shilingi Bilioni 143.15 kupitia ruzuku ya Serikali Kuu kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Afya ya Msingi ambapo hadi Februari, 2023 Shilingi Bilioni 124.10 zilipokelewa sawa na asilimia 86.69 ya fedha iliyoidhinishwa.

Waziri Kairuki alisema Shilingi Bilioni 69.95 ziliidhinishwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 15.15 ni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa kwa Zahanati 300, Shilingi Bilioni 47.70 kwa Vituo vya Afya 159 na Shilingi Bilioni 7.10 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba vya afya ya kinywa, meno na macho kwa Hospitali za Halmashauri 71 zilizokamilika na hadi kufikia Februari, 2023 jumla ya Shilingi Bilioni 54.55 zilikuwa zimepokelewa, sawa na asilimia 77.98.

Hadi Februari, 2023 Halmashauri zimekusanya jumla ya Shilingi Bilioni 625.31 sawa na asilimia 62 ya Makisio kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/23 ikiwa ni ongezeko la Shilingi Bilioni 9.70 sawa na asilimia 1.57 ikilinganishwa na Makusanyo ya Shilingi Bilioni 615.61 yaliyokusanywa kwa kipindi kama hiki katika Mwaka wa Fedha wa 2021/22.

"katika kuhakikisha kunakuwa na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imefanyia kazi changamoto zilizokuwepo katika mfumo wa mapato wa 'Local Government Revenue Collection Information System (LGRCIS)' kwa kusanifu na kujenga mfumo mpya wa TAUSI ambao umeanza kutumika katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23" alisema Kairuki.



# BUNGE LAPITISHA BAJETI YA OFISI YA RAIS - TAMISEMI YENYE JUMLA YA SHILINGI TRILIONI 9.1

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepitisha Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 yenye jumla ya Shilingi Trilioni 9.1.

Akitoa maelezo kuhusu hoja za Wabunge zilizojitokeza wakati wa kujadili Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI Bungeni Jijini Dodoma Aprili 18, 2023; Waziri Kairuki alisema katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi 2022/2023 Serikali iliidhinisha kiasi cha Shilingi Bilioni 280.35 kwa ajili ya ukamilishaji wa Maboma ya Vyumba vya Madarasa 8,252, Maabara 2,745, Mabwalo ya Chakula 86, Mabweni 433, Vituo vya Afya 52 na Zahanati 1,419 ambavyo utekelezaji wake kwa kiasi kikubwa umekamilika.

Waziri Kairuki aliendelea kufafanua kuwa katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24 Serikali imetenga jumla ya Shilingi Bilioni 20.56 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya Zahanati 376, Mabweni 10 na Bwalo la Chaklula 1 ambapo Serikali inaendelea kufanya tathmini ya mahitaji halisi ya maboma ambayo hayajakamilishwa na yale yanayoendelea kujengwa ili kuyawekea mpango wa kuyakamilisha kuwezesha utoaji bora wa huduma kwa wananchi.

Kwa upande wa Sekta ya Afya nchini, Waziri Kairuki alisema katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24 Serikali imetenga Shilingi Bilioni 116.92 kwa ajili ya Ununuzi wa Vifaa na Vifaa Tiba lakini pia Serikali itaendelea kununua Vifaa, Vifaa Tiba, Dawa na Vitendanishi kwa ajili ya Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Aidha, alisema Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari zitahakikisha maeneo yenye changamoto ya mtandao yanafikiwa ikiwa ni pamoja na kuendelea kuboresha mifumo iliyopo kama mfumo wa MUSE kwa Usimamizi na Matumizi ya Fedha za Umma, TAUSI kwa Ukusanyaji na Usimamizi wa Mapato, PlanRep kwa Mipango na Bajeti na Utoaji wa Taarifa za Halmashauri hali kadhalika mfumo wa FFARS katika Matumizi na Kuhasibu Fedha kwenye vituo vya kutolea huduma na vilevile kuendelea kutoa mafunzo kwa Watumishi wote wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI.



# BUNGE LAPITISHA BAJETI YA OFISI YA RAIS - TAMISEMI YENYE JUMLA YA SHILINGI TRILIONI 9.1







# SIFANYII KAZI VIMEMO AJIRA ZA UALIMU, AFYA: WAZIRI KAIRUKI

**Na Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Angellah Kairuki amesema ajira 21,000 za kada ya ualimu na afya watatenda haki na kwamba hatofanyia kazi vimemo vinavyotolewa na baadhi ya viongozi.

Pia amesema mtumishi yeyote wa Ofisi ya Rais TAMISEMI atakayebainika kuchukua rushwa au kufanya upendeleo wa aina yoyote katika kutoa ajira hizo atachukuliwa hatua kali za kinidhamu.

Kairuki ameyasema hayo bungeni wakati akihitimisha majadiliano ya bajeti ya wizara yake ya mwaka 2023/2024 tarehe 18 Aprili, 2023.

"Tutahakikisha zoezi hili linaenda kwa haki, wapo viongozi walionipigia simu na wengine kunitumia meseji wala sijajibu, tutatenda haki, bila hivyo tutawanyima haki watu wasiokuwa na viongozi wa kuwasemea, hata mimi nina ndugu zangu, lakini nimewambia waende kwenye mfumo rasmi," amesema.

"Hata kama kuna mtumishi Tamisemi atakayefanya vitendo vyovyote vya ukiukwaji haki atakwenda na maji, ndio maana kila siku natoa matangazo katika hili hakuna rushwa 25."

Aidha, amesema hoja ya walimu wanaojitolea serikali inatambua wapo walimu na watu wa afya wanaojitolea.

"Tunatambua uwepo wa walimu wanaojitolea kwa shule za msingi na sekondari, na uwepo wa walimu umesaidia kupunguza changamoto ya walimu katika baadhi ya maeneo nchini.

"Hadi sasa hatuna mfumo rasmi unaotumika kuwatambua wanaojitolea, baadhi ya walimu walikuwa wanapata nafasi ya kujitolea lakini wapo wanaotamani kuipata lakini wameikosa, hali kadhalika kwenye kada ya afya.

"Kukosekana kwa mfumo rasmi bado unaweka ombwe kati ya walimu na sekta ya afya na kituo ambacho wanajitolea. Tunaandaa mfumo wa kielekroniki utakaotusaidia kuwashughulikia watendaji hawa wanaojitolea," amesema.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Angellah Kairuki akihitimisha majadiliano ya bajeti ya OR- TAMISEMI bungeni Aprili 18, 2023.*

# DKT. MSONDE AELEKEZA MaDED WOTE NCHINI KULIPA MARA MOJA MADAI YOTE YA WALIMU

**Na. Mwandishi Wetu – Morogoro.**

Wakurugenzi wote wa Halmashauri za Wilaya, Miji, Majiji na Manispaa wameelekezwa kulipa mara moja madai yote ya Walimu ambao mpaka sasa hawajalipwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uhamisho kwani zoezi hilo pia lilifanyika ili kuboresha na kuimarisha utendaji kazi kwa dhima ya kuendelea kupaisha matokeo chanya ya Sekta ya Elimu nchini.

Wito huo umetolewa na Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde, alipokua akifungua Kikao Kazi cha Wadau kutoa maoni kuhusu kupitia Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu kinachofanyika Mkoani Morogoro kwa siku nne kuanzia Aprili 24, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Ualimu Morogoro (Kigurunyembe).



*Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde, akitoa hotuba ya kufungua Kikao Kazi cha Wadau kutoa maoni kuhusu kupitia Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu kinachofanyika Mkoani Morogoro kwa siku nne kuanzia Aprili 24, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Ualimu Morogoro (Kigurunyembe).*

“Ninatoa wito kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri za Wilaya, Miji, Majiji na Manispaa kulipa mara moja madai yote ya Walimu ambao mpaka sasa bado hawajalipwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uhamisho. Hatutaki Walimu wetu wawe



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba akitoa neno la utangulizi wakati wa ufunguzi wa Kikao Kazi cha Wadau kutoa maoni kuhusu kupitia Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu kinachofanyika Mkoani Morogoro kwa siku nne kuanzia Aprili 24, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Ualimu Morogoro (Kigurunyembe).*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa maelezo wakati wa ufunguzi wa Kikao Kazi cha Wadau kutoa maoni kuhusu kupitia Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu kinachofanyika Mkoani Morogoro kwa siku nne kuanzia Aprili 24, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Ualimu Morogoro (Kigurunyembe).*

# DKT. MSONDE AELEKEZA MaDED WOTE NCHINI KULIPA MARA MOJA MADAI YOTE YA WALIMU

na madai yoyote yale kwani mazoezi yote yaliyofanyika na kuleta madai hayo yalifanyika kwa dhamira njema ya Serikali katika kuendelea kuboresha na kuimarisha utendaji kazi kwa dhima ya kuendelea kupaisha matokeo chanya ya Sekta ya Elimu nchini." Alisema Dkt. Msonde

Aliongeza kuwa wale wote wanaohusika na mnyororo mzima wa ulipaji wa madeni hayo watekeleze na kutimiza wajibu wao kama inavyotakiwa ili kuondoa malalamiko na ya kulimbikiza madeni ya Walimu yasiyo na tija kwa Serikali na kuunga mkono juhudi kubwa za Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuiimarisha sekta hii ya elimu.

Aidha, Naibu Katibu Mkuu huyo akirejea mmomonyoko wa hivi sasa wa maadili nchini, alisisitiza Utatu katika malezi na maendeleo ya elimu kwa wanafunzi nchini akiwahusisha Wazazi, Walimu na Jamii kuwa ni muhimu sana katika kuwapatia weledi na maadili watoto wa Taifa la Tanzania kwa maendeleo chanya endelevu.

Dkt.Msonde alisema kuwa popote palipo na mazingira na elimu bora daima huleta matokeo chanya na bora na hivyo ni lazima elimu bora ipatikane kupitia kwa Walimu wa Taifa hili wenye mazingira bora na ili hilo liendelee kufanikiwa basi Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa eneo lake la majukumu iliyokasimiwa bado ina kazi kubwa ya kufanya katika kufikia matokeo haya.

Akiainisha sehemu ya mafanikio ambayo Serikali imeyapata kupitia TSC katika kipindi cha miaka miwili alisema, "Jumla ya Walimu 160,868 walipandishwa vyeo, Walimu 24,888 waliajiriwa na siku chache zilizopita hivi karibuni kibali cha ajira za Walimu 13,130 kimetolewa na Mhe. Rais ikiwa ni jitihada zake na dhamira yake ya dhati kuendelea kuimarisha elimu nchini."

Vilevile Dkt. Msonde alisema kutokana na kupitishwa na kuanza kutumika kwa Sera ya Elimu bila Malipo; mwaka 2021/2022 idadi ya wanafunzi iliongezeka mara mbili ya ile ya awali iliyotarajiwa na hivyo kusababisha Shule za Sekondari kutotosheleza idadi hiyo ya wanafunzi na Serikali kutenga zaidi ya Shilingi Bilioni 300 zilizojenga shule kote nchini na kutosheleza mahitaji.

"Katika jitihada hizo Serikali kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha uliopita ilitenga jumla ya Shilingi Bilioni 160 kujenga madarasa mengine zaidi baada ya kuonekana kuongezeka kwa wanafunzi zaidi wanaotakiwa kujiunga na masomo jambo lililoashiria mwamko zaidi wa jamii katika kupata elimu kutokana na kuimarika kwa mazingira na Sekta nzima ya elimu nchini." Alisema Naibu Katibu Mkuu

Akielezea miradi inayoendelea kupitia Wadau wa Maendeleo katika Sekta ya Elimu nchini, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka OR-TAMISEMI, Dkt. Msonde alisema Mradi wa SEQUIP umetenga jumla ya Shilingi Trilioni 1.2 katika kuboresha sekta hiyo huku huku jumla ya Shule 1,026 zikijengwa kote nchini, Shule 232 za Kata zilizo karibu zaidi na wananchi





*Baadhi ya washiriki wa Kikao Kazi cha Wadau kutoa maoni kuhusu kupitia Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu kinachofanyika Mkoani Morogoro kwa siku nne kuanzia Aprili 24, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Ualimu Morogoro (Kigurunyembe) wakiwa katika hali ya utulivu wakati wa kikao.*

# DKT. MSONDE AELEKEZA MaDED WOTE NCHINI KULIPA MARA MOJA MADAI YOTE YA WALIMU



*Mmoja wa washiriki wa Kikao Kazi cha Wadau kutoa maoni kuhusu kupitia Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu kinachofanyika Mkoani Morogoro kwa siku nne kuanzia Aprili 24, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Ualimu Morogoro (Kigurunyembe) akichangia mada wakati wa kikao.*

zimejengwa, Shule 26 za Bweni kwa Wasichana zinajengwa huku jumla ya Shule 184 ikiwa ni shule moja katika kila Halmashauri zimeidhinishwa zijengwe huku Shule 10 kati ya hizo zikielekea kwenye ukamilifu.

Akizungumzia Mradi wa BOOST, Dkt. Msonde alisema jumla ya Shilingi Trilioni 1.15 zimetengwa kwa kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wake ambao umelenga kuboresha na kuimarisha Elimu Msingi na Awali ikiwa ni pamoja na kujenga Shule za Msingi 302, Madarasa 3,338 na Nyumba za Walimu 41.

Akimkaribisha Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba alisema wadau walioshirikishwa ni katika kikao kazi hicho ni sehemu ya uwakilishi kutoka Wizara, Taasisi za Serikali na Taasisi zisizokuwa za Serikali ambazo kwa namna moja au nyingine zinamgusa Mwalimu.

Prof.Komba alisema kuwa Tume ina imani kubwa sana kupitia uwakilishi huo itaweza kuwa na andiko ambalo litabeba maudhui ambayo yatatoa mwelekeo kwa Serikali wa namna bora ya kusimamia Utumishi wa Walimu.

Naye Katibu na Mtendaji Mkuu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama alitoa maelezo ya awali ya Kikao Kazi hicho alisema Tume imeandaa kikao hicho cha Wadau kwa siku nne kwa ajili ya kupata maoni na mtazamo kuhusu namna bora ya kusimamia Utumishi wa Walimu kwani wadau walioshirikishwa ni dhahiri kuwa ni watu mahiri wenye taaluma na uzoefu wa kutosha.

Tume ya Utumishi wa Walimu imeundwa kwa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448, na ilianza kutekeleza majukumu yake rasmi Julai 01, 2016 ikiwa ni Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari waliopo kwenye Utumishi wa Umma Tanzania Bara.



*Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde (katikati) katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki wa Kikao Kazi cha Wadau cha kutoa maoni kuhusu kupitia Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu kinachofanyika Mkoani Morogoro. Pichani, wa pili kutoka kushoto ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba na wa pili kutoka kulia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.*










*Matukio mbalimbali wakati wa Kikao Kazi cha Wadadukutoa maoni kuhusu kupitia Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu kinachofanyika Mkoani Morogoro kwa siku nne kuanzia Aprili 24, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Ualimu Morogoro (Kigurunyembe).*









*Matukio mbalimbali wakati wa Kikao Kazi cha Wadadukutoa maoni kuhusu kupitia Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu kinachofanyika Mkoani Morogoro kwa siku nne kuanzia Aprili 24, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Ualimu Morogoro (Kigurunyembe).*

# TSC MISSENYI YAWAJENGEA UWEZO WALIMU WA KATA ZA KANYIGO, KASHENYE NA MINZIRO

Tume ya Utumishi wa Walimu imewajengea uwezo zaidi ya walimu 106 katika kata za Kanyigo, Kashenye na Minziro juu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu kwa lengo la kuwawezesha walimu kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu.









*Picha mbalimbali zikionesha kikao kazi kati ya TSC Wilaya ya Missenyi na Walimu wa Kata za Kanyigo, Kashenye na Minziro kilicholenga kuwajengea uwezo walimu juu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu.*

# TSC YAANZA KUFANYA TATHMINI YA HALI YA WALIMU WA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI ZA SERIKALI

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Kifungu cha (5) (d) cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Na.25 ya Mwaka 2015 kimeipa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) jukumu la kusimamia uwiano wa usambazaji wa Walimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Shule.

Katika kutekeleza jukumu hilo, Mwezi Novemba, 2021 TSC kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI ilifanya zoezi la kukusanya, kuchambua na kuhakiki taarifa za walimu waliopo, wanaohitajika pamoja na upungufu katika shule za Msingi na Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Uchambuzi wa taarifa hizo ulionesha kuwa, jumla ya walimu waliokuwepo ni 258,291 ambapo kati yao walimu wa shule za Msingi ni 173,591 na Walimu wa shule Sekondari walikuwa 84,700 huku taarifa hiyo ikibainisha kuwa mahitaji halisi ya ilikuwa ni walimu 473,915.

Baada ya taarifa ya zoezi hilo Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kukabiliana na upungufu wa walimu ambapo kwa nyakati tofauti vibali vya ajira vimetolewa na walimu wameendelea kuajiriwa.

Kwa kuwa tangu wakati tathmini hiyo ilipofanyika hadi sasa, yapo mabadiliko kwa baadhi ya walimu kuhitimisha utumishi wao kwa sababu mbalimbali ikiwemo kustaafu, kufariki, kufukuzwa au kuacha kazi, TSC imeamua kufanya tathmini ya kina kujua hali halisi ya idadi ya walimu kwa sasa.

Kazi hiyo ambayo imeanza kufanyika mwezi Aprili, 2023 inalenga kuiwezesha Tume kuwa na taarifa sahihi kuhusu hali ya walimu nchini, (waliopo, mahitaji na upungufu / ziada) ili kuishauri Serikali katika kutoa maamuzi sahihi kwa ajili ya kuboresha usimamizi wa Elimu nchini.






*Watendaji kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu pamoja na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wakiwa katika kikazo kazi cha kufanya tathmini ya walimu nchini. Kikao kazi hicho kimefanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

# DK. MSONDE AFANYA ZIARA YA KUSHTUKIZA SHULE YA MSINGI KIGURUNYEMBE, AINGIA MOJA KWA MOJA DARASANI

**Na Mwandishi Wetu – Morogoro.**

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR–TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde tarehe 24 Aprili, 2023 amefanya ziara ya kushtukiza katika shule ya Msingi Kigurunyembe iliyopo katika Manispaa ya Morogoro ambapo alikwenda moja kwa moja darasani kujionea umahiri wa wanafunzi katika masomo wanayofundishwa.

Naibu Katibu Mkuu huyo alitembelea darasa la saba, la sita na la tatu ambapo katika madarasa hayo alitaka kuona umahiri wa wanafunzi hao katika kujieleza kwa lugha ya kiingereza.

Baada ya kuwahoji na kusikiliza namna wanafunzi hao wanavyojieleza, Dkt. Msonde alionesha kuridhishwa na kiwango cha ujuzi wa wanafunzi hao huku akiwapongeza walimu wa shule hiyo kwa kufanya kazi kwa bidii, weledi na uzalendo. Naibu Katibu Mkuu huyo alisema juhudi hizo zinaunga mkono jitihada za Serikali za kufanya maboresho katika sekta ya elimu katika kuhakikisha wanafunzi wanapata ujuzi na umahiri katika masomo wanayofundishwa.

"Kama tunavyoona walimu wetu wanafanya kazi kubwa, kumsimamia mwanafunzi wa darasa la tatu hadi kuwa na uwezo mzuri wa kujieleza namna hii, siyo kazi ndogo. Na hii siyo kwa shule hii peke yake, ukienda shule yoyote ya msingi utaona namna walimu wanavyojitoa kufundisha wanafunzi. Hivyo, tunafarijika sana kuona walimu wetu wana mwitikio chanya katika kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuboresha elimu," alisema.

Pamoja na kuwawezesha wanafunzi kupata ujuzi na maarifa, Dkt. Msonde amesema walimu wana jukumu la malezi kwa watoto ambapo wanatakiwa kuwafundisha tabia njema, uzalendo na nidhamu ili kujenga taifa la watu waadilifu wanaoipenda nchi yao.

Hata hivyo, ameeleza kuwa jukumu la malezi kwa watoto haliwezi kusimamiwa na mwalimu peke yake bali wazazi/walezi, viongozi wa siasa na dini na jamii kwa ujumla wana wajibu wa kushirikiana na mwalimu ili kusaidia watoto kukua katika maadili mema yanayozingatia utamaduni wa kitanzania.

Katika ziara hiyo, Dkt. Msonde aliambatana na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba, Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama, Katibu Tawala Msaidizi (Elimu) wa Mkoa wa Morogoro, Germana Mung'aho pamoja na watendaji wengine wa TSC ambao wapo mkoani Morogoro kwa ajili ya kikao kazi cha wadau kinacholenga kupata maoni kuhusu kupitia sheria na kanuni zote zinazosimamia utumishi wa walimu.



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde (mwenye tai) akiongea na wanafunzi darasani wakati alipofanya ziara ya kushtukiza katika shule ya Msingi Kigurunyembe iliyopo katika Manispaa ya Morogoro tarehe 24 Aprili, 2023.*



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde akiongea na wanafunzi darasani wakati alipofanya ziara ya kushtukiza katika shule ya Msingi Kigurunyembe iliyopo katika Manispaa ya Morogoro tarehe 24 Aprili, 2023.*

# DK. MSONDE AFANYA ZIARA YA KUSHTUKIZA SHULE YA MSINGI KIGURUNYEMBE, AINGIA MOJA KWA MOJA DARASANI



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde (mwenye tai) akiongea na mwanafunzi darasani wakati alipofanya ziara ya kushtukiza katika shule ya Msingi Kigurunyembe iliyopo katika Manispaa ya Morogoro tarehe 24 Aprili, 2023. Katikati ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba na kushoto ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.*





*Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama akiongea na wanafunzi darasani wakati wa ziara ya Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde katika shule ya Msingi Kigurunyembe iliyopo katika Manispaa ya Morogoro tarehe 24 Aprili, 2023.*



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde (mwenye tai) akitoa zawadi kwa wanafunzi baada ya kujieleza vizuri kwa lugha ya kiigereza wakati wa ziara yake katika shule ya Msingi Kigurunyembe iliyopo katika Manispaa ya Morogoro tarehe 24 Aprili, 2023.*



*Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama akiwa na wanafunzi darasani wakati wa ziara ya Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde katika shule ya Msingi Kigurunyembe iliyopo katika Manispaa ya Morogoro tarehe 24 Aprili, 2023.*

# DK. MSONDE AFANYA ZIARA YA KUSHTUKIZA SHULE YA MSINGI KIGURUNYEMBE, AINGIA MOJA KWA MOJA DARASANI







*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde akiongea na wanafunzi darasani wakati alipofanya ziara ya kushtukiza katika shule ya Msingi Kigurunyembe iliyopo katika Manispaa ya Morogoro tarehe 24 Aprili, 2023.*


OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)
Kila la Kheri
Kidato cha Sita
Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tunawatakia Kila la Kheri Wanafunzi wa kidato cha sita wote katika Mitihani yao ya Taifa itakayoanza 02/05/2023.
www.tsc.go.tz
secretary@tsc.go.tz
Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

# WATUMISHI TSC WAPATA MAFUNZO YA ZIMAMOTO

**Na Mwandishi wetu – Dodoma.**

Watumishi wa Tume ya Utumishi wa walimu (TSC) wamepatiwa Mafunzo ya Zimamoto na Ulinzi wa Mali wakati wa majanga ya moto ili kuweza kujilinda pale majanga ya moto yanapotokea.

Mafunzo hayo yalitolewa na Maafisa wa Jeshi hilo kutoka Ofisi za Zimamoto Makao Makuu – Dodoma tarehe 17 Aprili, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni jijini Dodoma.














*Mafunzo ya Zimamoto na Ulinzi wa Mali wakati wa majanga ya moto yakiwa yanaendelea.*


OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)
Kheri ya Siku ya
Muungano
APRILI, 26
Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tunawatakia Kheri Watanzania wote kwa kutimiza Miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.
Tume Utumishi wa Walimu Tanzania
www.tsc.go.tz

# TSC UKEREWE WATOA MAFUNZO KWA WALIMU KATA YA NAMILEMBE

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ukerewe imetoa mafunzo kwa walimu wa Kata ya Namilembe yaliyolenga kutoa elimu juu ya Sheria, Kanuni na taratibu za Utumishi wa Walimu ili kuwawezesha walimu kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Miiko na maadili ya taaluma hiyo.





*Wanafuzi wa Shule ya Sekondari Busangumugu wakimsikiliza Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ukerewe, Mwl. Stephen Kushoka (kulia) na Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC Ukerewe, Mwl. Magreth David mara baada ya kutoa mafunzo kwa walimu wa kata ya Namilembe yaliyofanyika tarehe 19 Aprili, 2023.*




*Picha ya pamoja kati ya Maafisa wa TSC Wilaya ya Ukerewe na Walimu wa Kata ya Namilembe mara baada ya kumaliza mafunzo yaliyolenga kujenga uelewa juu ya masuala mbalimbali ya Utumishi wa Walimu. Mafunzo hayo yalifanyika tarehe 19 Aprili, 2023 katika shule ya Sekondari Busangumugu.*

# MKUU WA WILAYA YA IRAMBA ATIMIZA AHADI YAKE KWA WALIMU KUTEMBELEA MBUGA YA WANYAMA NGORONGORO




**Na. Mwandishi Wetu – Ngorongoro, Arusha.**

Mkuu wa Wilaya ya Iramba Mkoani Singida, Suleimani Yusuph Mwenda, ametimiza ahadi yake aliyoitoa kwa Walimu wa Shule ya Sekondari Lulumba na Tumaini Wilayani Iramba baada ya kufanya vizuri kwenye Mitihani ya Kidato cha Sita kwa Mwaka 2022 baada ya Shule hizo kuibuka kidedea kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa.

Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kupitia Idara ya Elimu Sekondari ulitekeleza ahadi hiyo ya Mkuu wa Wilaya ya Iramba Mkoani Singida Suleimani Yusuph Mwenda aliyoitoa kwa vipindi viwili tofauti alipohudhuria Siku ya Elimu Shule ya Sekondari Lulumba pamoja na Siku ya Elimu Shule ya Sekondari Tumaini iliyofanyika Mwaka 2022 kwa kutoa ahadi hiyo ya kuwapeleka kupumzika kwenye mbuga yoyote watakayoichagua.

Kwa ahadi hiyo ya Mkuu wa Wilaya, Walimu hao walitembelea mbuga hiyo kwa lengo la kwenda kutalii na kupumzika ikiwa pia ni sehemu ya kuongeza hamasa ya utalii wa ndani ya nchi kutokana na shule zao kufanya vizuri mfululizo kwenye matokeo ya mitihani ya Kidato Cha Sita.

Katika ziara hiyo ya kutembelea Mbuga ya Wanyama ya Ngorongoro; Walimu 17 wa Shule za Sekondari za Lulumba na Tumaini waliongozana na Maafisa watatu kutoka Idara ya Elimu Sekondari na Wakuu wa Shule za Sekondari 25 ili kuongeza hamasa zaidi katika uwajibikaji wa pamoja na kuleta tija kwa Wilaya, Mkoa na Taifa kwa ujumla.





# MKUU WA WILAYA YA IRAMBA ATIMIZA AHADI YAKE KWA WALIMU KUTEMBELEA MBUGA YA WANYAMA NGORONGORO







# MAABARA YA TEHAMA YAZINDULIWA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIMBIJI

**Na. Mwandishi Wetu – Dar Es Salaam.**

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) leo tarehe 19/4/2023 amezindua rasmi maabara ya TEHAMA yenye vifaa vya kielektroni vilivyotolewa na nchi ya Korea kupitia mradi wa KLIC 2022 (Korean E-Learning Improvement Cooperation 2022) katika shule ya Sekondari Kimbiji iliyopo wilaya ya Kigamboni Jijini Dar es salaam.

Katika halfa fupi ya uzinduzi wa maabara hiyo Dkt. Aneth amewataka walimu kutumia vyema teknolojia hiyo katika kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji hasa katika masomo ya sayansi.

Aidha,amewaasa walimu kuwaruhusu wanafunzi kutumia maabara hiyo kutafuta maarifa yatakayowasaidia kupata ujuzi mbalimbali.

"Walimu muwaruhusu wanafunzi kutumia vifaa hivyo vya kieletroni ili kurahisisha ujifunzaji na upatikanaji wa maarifa mbalimbali yatakayowasaidia



*Picha ya pamoja ya Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ukerewe, Mwl. Stephen M. Kushoka na walimu walioshiriki kikao kazi cha kuelimisha walimu juu ya Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma.*

wanafunzi kuwa na ujuzi, lengo la maabara hii ni kuleta matokeo chanya katika shule hii" amesema Dkt.Komba.

Aidha,amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuboresha sekta ya Elimu nchini.

Awali, Dkt.Komba alikabidhi vishkwambi kwa walimu 20 waliohitimu programu ya mafunzo ya KLICK 2022 yaliyotolewa na nchi ya Korea kwa kushirikiana na TET.

Kwa upande wake , Mwalimu Mkuu wa shule ya Sekondari Kimbiji Bi.Joyce Ndaona ameishukuru serikali kupitia TET kwa mafunzo hayo pamoja na vifaa vilivyotolewa ambapo amesema vitasaidia katika ufundishaji na ujifunzaji.

Mwenyekiti wa kamati ya shule hiyo Bwana Joseph Njoka amesema muda tulionao sasa ni wa kiteknolojia hivyo upatikanaji wa vifaa hivyo ni motisha kwa walimu na kuahidi vitalindwa na kutenda kazi iliyokusudiwa katika kuleta matokeo chanya kwa shule.

Vifaa vilivyokabidhiwa katika maabara hiyo ni pamoja na "UPS 26,computure Monitor 25, system Unit 25,Wirless keyboard 35,projector moja, scanner moja,printer moja, wireless mouse 35, headphone 25, electric blackboard moja ,webcamera 26,digital podium moja,wired keyboard 25, ,wired mouse 25,speaker 26,adapter 49 na usb flash disk 50"





# REDEOA WAMPA TUZO RAIS SAMIA KWA KULETA MAPINDUZI KATIKA SEKTA YA ELIMU NCHINI

- *Amefanikisha kuandikishwa kwa Wanafunzi wa Awali 1,500,227 (109%), Darasa la Kwanza 1,767,586 (108%) na Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza walioripoti 1,002,093 (93%);*
- *Mafanikio mengine ni pamoja na Ujenzi wa Vyumba vya Madarasa 8,000 na Mabweni 79;*
- *Kununuliwa na kusambazwa kwa magari ya Elimu Mikoa na Halmashauri, Pikipiki za Maafisa Elimu Kata na Vishikwambi kwa Walimu wote nchini ili kurahisisha ufuatiliaji na usimamizi wa elimu nchini.*

**Na. Mwandishi Wetu – Mwanza.**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amepatiwa Tuzo Maalum kwa ajili ya kuleta Mapinduzi katika Sekta ya Elimu nchini Tanzania.

Hafla ya kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ilifanyika Aprili 05, 2023 Jijini Mwanza ambapo Umoja wa Maafisa Elimu wa Mikoa na Halmashauri (REDEOA) walimtunuku Tuzo hiyo maalum ambayo ilipokelewa na Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kutambua mchango wake mkubwa wa kusimamia, kuipaisha na kupelekea mapinduzi makubwa ya elimu nchini.

Katika hafla hiyo Waziri Kairuki aliwataka Viongozi wa Elimu nchini kutokuchoka kusimamia na kuyasemea masuala ya elimu kwani wao ndio waliopewa dhamana na Watanzania.

Kairuki alisema njia pekee ya kumsaidia Mheshiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, nikwa kusimamia kwa weledi Sekta ya Elimu ambapo aliwataka Viongozi hao kudumisha ushirikiano na Wananchi pamoja na kuwawajibisha Viongozi wa elimu wanaoshindwa kutimiza wajibu wao.

"Kila Afisa Elimu wa Mkoa na Halmashauri ahakikishe anadumisha ushirikiano na Wananchi na Wadau wote wa elimu, anasimamia ufundishaji na ujifunzaji, Wanafunzi wenye mahitaji maalum wanaendelea kusaidiwa kwa ukaribu na kusimamia vema Miradi ya Maendeleo katika Sekta ya Elimu na Viongozi wanaoshindwa kutimiza wajibu wao wachukuliwe hatua bila kuwaonea na bila kuchelewa." Alisema Kairuki.

Katika Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Sekta ya Elimu chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI imefanikiwa kuandikisha Wanafunzi wa Awali 1,500,227 (109%), Darasa la Kwanza 1,767,586 (108%) na Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza walioripoti wakiwa 1,002,093 (93%).

Kwa mujibu wa Waziri Kairuki mafanikio mengine ni pamoja na Ujenzi wa Vyumba vya Madarasa 8,000 vilivyojengwa kwa Shilingi Bilioni 160 ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi 1,076,402 waliofaulu na wote kuchaguliwa kwenda shuleni.

Aidha, kupitia Mradi wa GPE LANES mabweni 20 yalijengwa kwa Shilingi Bilioni 2, Mabweni 50 Shilingi Bilioni 4 kwa Mradi wa TCRP 5441 na Mabweni tisa (9) yalijengwa kwa Shilingi Milioni 960 kwa fedha za Uhuru mwaka 2022.

Naye Mwenyekiti wa REDEOA, Germana Mng'ao, aliishukuru Serikali kwa kurahisisha ufuatiliaji na usimamizi wa elimu nchini baada ya kupokea magari kwa ajili ya Mikoa na Halmashauri, Pikipiki za Maafisa Elimu Kata na Vishikwambi kwa Walimu wote nchini.

Katika hafla hiyo mada mbalimbali ziliwasilishwa ikiwa ni Pamoja na kutolewa kwa Tuzo nyingine kwa Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kwa kusimamia Sekta ya Elimu vizuri, Naibu Katibu Mkuu (ELIMU), Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Dkt. Charles Msonde, Mkurugenzi wa Elimu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mwl. Vicent Kayombo, Mwenyekiti wa REDEOA Germana Mng'ao na Afisa Elimu wa Mkoa wa Pwani, Sarah Mlaki.



# SERIKALI YAWAASA VIONGOZI WA ELIMU KUFUATILIA VITENDO VYA UKATILI SHULENI

**Na. Mwandishi Wetu – Mwanza.**

Serikali imewataka Maafisa Elimu wa Mikoa na Halmashauri nchini kufuatilia vitendo vya ukatili vinavyofanywa shuleni ili kuboresha mazingira salama, rafiki na wezeshi kwa Watoto.

Kauli hiyo ya Serikali ilitolewa Aprili 3, 2023 Jijini Mwanza na Dkt. Lyabwene Mtahabwa, Kamishna wa Elimu wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Umoja wa Maafisa Elimu wa Mikoa na Halmashauri Tanzania Bara (REDEOA) ambaye alimwakilisha Prof. Adolf Mkenda (Mb), Waziri wa Elimu, Sayani na Teknolojia.

Dkt. Mtahabwa alisema Sekta ya Elimu inakabiliwa na changamoto ya mmomonyoko wa maadili, uwajibikaji hafifu na ukatili kwa watoto ambapo tafiti zinaonyesha kuwa asilimia 60 ya ukatili unatokea nyumbani na asilimia 40 unatokea shuleni.

"Zipo baadhi ya changamoto zinazoweza kuathiri juhudi za Serikali katika kutoa Elimu Bora kama vile kumomonyoka kwa maadili kwa baadhi ya jamii, vitendo vya ukatili kwa watoto nje na ndani ya shule, uwajibikaji hafifu kwa baadhi ya Watumishi katika Sekta ya Elimu." Alisema Dkt. Mtahabwa.

Dkt. Mtahabwa alisema watoto hawapati haki ya kupata likizo, hawapewi kazi za mikono ili waweze kujitegemea ambapo katika hilo aliwataka Viongozi hao kusimamia ushirikiano wa jamii na shule ili kuleta mabadiliko ya elimu kote nchini.

Akitoa neno la ukaribisho kwa Mgeni Rasmi, Dkt. Charles Msonde, Naibu Katibu Mkuu (ELIMU), Ofisi ya Rais – TAMISEMI, alisema baadhi ya shule zimekuwa na changamoto ya kukosa wanafunzi wanaojiunga na Darasa la Tano lakini pia kuwepo kwa wanafunzi asilimia 71 waliojiunga na kidato cha kwanza mwaka 2022 kukosa umahiri wa somo la kiingereza hali iliyopelekea kuandaa Mkakati Maalum wa kufundishia wenye vigezo 22 ikiwa ni pamoja na kuimarisha Ufundishaji wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa Darasa la Kwanza na pia kuimarisha ufundishaji wa Darasa la Tatu.

Naye Mwenyekiti wa REDEOA Bi. Germana Mng'ao, aliishukuru Serikali kwa kupeleka Miradi ya kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia ya BOOST (Shule za Msingi) na SEQUIP (Sekondari), kuwajengea uwezo Walimu wa Sekondari zaidi ya 13,000 na kuwapatia Walimu vishikwambi nchi nzima kuimarisha ufundishaji.



# TSC YATAKIWA KUENDELEA KUSHUGHULIKIA KERO NA MALALAMIKO YA WALIMU



*Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Fatma Abubakar Mwassa akitoa hotuba kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Angellah Jasmine Kairuki wakati wa kufunga kikao kazi cha kupitia Sheria na Kanuni zote zinazosimamia mzunguko wa utumishi wa mwalimu tarehe 27 Aprili, 2023.*



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba akitoa neno la utangulizi wakati wa kufunga Kikao Kazi cha Wadau kutoa maoni kuhusu kupitia Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu tarehe 27 Aprili, 2023 mkoani Morogoro katika Ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Ualimu (Kigurunyembe).*

**Na Mwandishi wetu – Morogoro.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeagizwa kuendelea kufuatilia na kuhakikisha walimu wote wenye malalamiko na kero mbalimbali wanapatiwa ufumbuzi kwa haraka na kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ili waendelee kufanya kazi kwa amani na utulivu.

Alisema ili kuwa na elimu bora ni lazima walimu wawezeshwe kutekeleza majukumu yao vizuri ikiwa ni pamoja na katutua kero zinazowakabili zikiwemo ueleweshaji wa upandishaji madaraja, kutolipwa madai mbalimbali kwa wakati, kutobadilishiwa kazi/cheo kwa wakati baada ya kujiendeleza na kusisitiza kuwa endapo changamoto hizo zitaendelea kujitokeza ni rahisi kwa walimu kukata tamaa.

Agizo hilo limetolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Angellah Jasmine Kairuki katika hotuba yake iliyowasilishwa na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Fatma Abubakar Mwassa wakati wa kufunga kikao kazi cha wadau kilicholenga kufanya mapitio ya sheria na kanuni zote zinazosimamia mzunguko wa mwalimu ili kutoa mwelekeo wa usimamizi bora wa utumishi wa walimu nchini kilichofanyika tarehe 27 Aprili, 2023 mjini Morogoro.

"Walimu wanafanya kazi kubwa katika nchi hii, licha ya jukumu la kufundisha darasani ukienda vijijini utakuta wao ndio wanasuluhisha migogoro ya ndoa, ya ardhi nk, ndio wanaotegemewa kutoa ushauri bora kwa wanajamii na mambo mengine mengi wanayofanya. Hivyo, ni lazima tuwahemu walimu kwa kuhakikisha maslahi yao yanazingatiwa kikamilifu."

"Kwa kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu ndiyo iliyopewa dhamana ya kusimamia utumishi wa mwalimu tangu anapoajiriwa hadi anapohitimisha utumishi wa umma, natumia fursa hii kuwaagiza kufuatilia na kuhakikisha walimu wote wenye malalamiko na kero mbalimbali, kero zao zinapatiwa ufumbuzi kwa haraka na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu," alisema.

Sambamba na hilo, Waziri ameiagiza TSC kwa kushirikiana na Halmashauri kuweka namna bora ya walimu kupata mafunzo wakiwa kazini ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi huku akieleza kuwa ili mwalimu aweze kutoa matunda mazuri ni muhimu kupatiwa mafunzo ya mara kwa mara.

Ameongeza kuwa ni muhimu kwa Halmashauri kutenga

# TSC YATAKIWA KUENDELEA KUSHUGHULIKIA KERO NA MALALAMIKO YA WALIMU



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa maelezo wakati wa kufunga Kikao Kazi cha Wadau kutoa maoni kuhusu kupitia Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu tarehe 27 Aprili, mkoani Morogoro katika Ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Ualimu Morogoro (Kigurunyembe).*



*Mtaalamu wa elimu kutoka Benki ya Dunia ambayo inafadhili Mradi wa BOOST, Gema Todd akitoa salamu kutoka Benki ya Dunia wakati wa kufunga kikao kazi cha kupitia Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu tarehe 27 Aprili, 2023 katika chuo cha ualimu Morogoro kilichopo Manispaa ya Morogoro.*

bajeti kila mwaka kwa ajili ya mafunzo ya walimu ili angalau kila mwaka wawepo walimu kadhaa wanaowezeshwa kupata mafunzo huku akiielekeza TSC kusaidia kutoa elimu kwa walimu juu ya mafunzo wanayopaswa kupata ili kuongeza ubora katika ufundishaji.

Aidha, ameagiza Tume kuhakikisha inatoa elimu kwa walimu wapya 13,130 watakaoajiriwa hivi karibuni kabla hawajanza kufundisha ili watambue miiko na maadili ya kazi ya ualimu kwa lengo la kuwasaidia kujiepusha na vitendo vya ukiukwaji wa maadili ya utumishi wa walimu.

"Serikali yetu kupitia Rais wetu mpendwa inajitahidi kuhakikisha inaimarisha elimu, hata hivyo mafanikio ya azma hii yatategemea pia kuwepo kwa walimu wanaojituma na wenye uadilifu. Natambua Tume ya Utumishi wa Walimu inasimamia suala zima la maadili kwa walimu, hivyo tuendelee kuelimisha na kusimamia maadili yao ipasavyo. Aidha, kwa walimu wapya 13,130 watakaoajiriwa hivi karibuni mhakikishe mnawaelimisha kuhusu Maadili na Miiko ya kazi ya ualimu kabla ya kuripoti vituoni na kuanza kazi ya malezi kwa watoto wetu," amesema.

Akitoa neno la kumkaribisha Mkuu wa Mkoa, Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba amesema kuwa Kikao kazi hicho kilihusu wadau waliobobea katika msuala ya sheria, elimu na usimamizi wa rasilimali watu na kimechambua mambo mbalimbali yanayomhusu mwalimu na kutoa mwelekeo bora zaidi wa usimamizi wa mwalimu na utakaomsaidia kuhudumiwa kwa ufanisi zaidi.

"Wadau walioko mbele yako ni uwakilishi kutoka Wizara/Taasisi za Serikali na Taasisi zisizokuwa za Serikali ambazo kwa namna moja au nyingine zinamgusa mwalimu. Ni imani yangu kuwa kupitia uwakilishi huu tumeweza kuwa na andiko ambalo limebeba maudhui ambayo yatatoa mwelekeo na ushauri kuhusu namna bora ya kusimamia utumishi wa mwalimu. Hivyo kwa siku hizi nne (24 – 27 Aprili, 2023) tumetumia uzoefu na elimu Mungu aliyotujalia katika kufanikisha jukumu hilo muhimu," amesema Prof. Komba.

Kwa upande wake Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama alisema Mhe Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya kazi kubwa ya kuboresha sekta ya elimu ikiwemo ujenzi wa madarasa kuanzia elimu ya awali, Msingi na Sekondari nchi nzima, kupitia Sera ya Elimu bila malipo madarasa 3,000 kwa Shule za Msingi yamejengwa, kupitia Mradi wa SEQUIP ambao umelenga kuboresha elimu ya

# TSC YATAKIWA KUENDELEA KUSHUGHULIKIA KERO NA MALALAMIKO YA WALIMU




*Baadhi ya washiriki wa Kikao Kazi cha Wadau kutoa maoni kuhusu kupitia Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu kilichofanyika Mkoani Morogoro kwa siku nne kuanzia Aprili 24, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Ualimu Morogoro (Kigurunyembe) wakiwa katika hali ya utulivu wakati wa kufunga kikao kazi hicho.*

Sekondari, Shule za Sekondari 1,026 zinajengwa ambapo kati ya shule hizo 282 zimejengwa ngazi ya Kata, shule 10 kati ya 26 za bweni kwa wasichana zimejengwa. Aidha, jumla ya shule 184 ikiwa ni shule moja katika kila Halmashauri zimeidhinishwa zijengwe.

"Serikali imeweza kuwa na mradi wa BOOST ambao umelenga kuimarisha elimu ya Msingi nchini. Mradi huo ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia, Serikali yetu imepokea kiasi cha shilingi za kitanzania Trilioni 1.15 kwa ajili ya kuimarisha elimu ya Awali na Msingi nchini. Hata kikao kazi kilichofanyika kwa siku nne katika ukumbi huu ni uwezesho wa fedha za Mradi huo. Naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru kwa dhati Wadau wetu wa Maendeleo wa Benki ya Dunia ambao kupitia Mradi wa BOOST wamewezesha kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kuboresha elimu nchini," alisema Nkwama.

Katibu huyo aliongeza kuwa TSC ni miongoni mwa watekelezaji wa shughuli za Mradi wa BOOST ambapo katika shughuli zilizolengwa kutekelezwa na Mradi huo ni pamoja na kuhuisha Sheria na Kanuni zote zinazohusu mzunguko wa Utumishi wa Mwalimu kwa ajili ya kuandaa utaratibu wa kumhudumia mwalimu ambapo Tume katika hatua za awali za utekelezaji wa shughuli hiyo, Tume iliunda kikosi kazi cha wa masuala ya sheria, elimu na Utumishi kutoka ofisi mbalimbali za Serikali

"Timu hiyo iliundwa na wataalamu kutoka Ofisi ya Rais Ikulu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikli za Mitaa, Wizara ya Elimu na Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, TSC na Chuo Kikuu cha DodomaOR- Ikulu, OR- UTUMISHI, OR- TAMISEMI, WyEST, AG, TSC na Chuo Kikuu cha UDOM. Timu hiyo ndiyo iliyotengeneza rasimu ya andiko ambayo imepitiwa na Kikao cha wadau waliopo mbele yako," alisema.

Naye mtaalamu wa elimu kutoka Benki ya Dunia ambayo ndio yenye Mradi wa BOOST ambao unaofadhili kazi hiyo, Gema Todd amesema Benki ya Dunia inaridhishwa na namna kazi hiyo ya kufanya mapitio ya sheria na kanuni zote zinazohusu mwalimu na kutoa mwelekeo wa namnabora ya kumsimamia mwalimu inavyotekelezwa kwa ufanisi na TSC.

"Kwa niaba ya Benki ya Dunia ninaipongeza TSC kwa namna inavyosimamia kazi hii. Tumefikia hatua hii nzuri kwa kufanya kazi kwa pamoja, tumesikilizana vizuri na tumeelewana. Wote lengo letu limekuwa kumwangalia mwamu, kuona kuwa ni nini tufanye ili mwalimu huyu aweze kutekeleza majukumu yake katika namna bora zaidi bila kuwa na vikwazo," amesema Todd.

# TSC YATAKIWA KUENDELEA KUSHUGHULIKIA KERO NA MALALAMIKO YA WALIMU



*Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Fatma Mwassa (katikati) katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa Menejimenti na Kamishna wa TSC walioshiriki Kikao Kazi cha Wadau cha kutoa maoni kuhusu kupitia Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu kilichofanyika Mkoani Morogoro. Pichani, wa pili kutoka kushoto ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba na wa pili kutoka kulia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.*



*Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Fatma Mwassa (katikati) katika picha ya pamoja na baadhi ya ajumbe wa Menejimenti na Kamishna wa TSC walioshiriki Kikao Kazi cha Wadau cha kutoa maoni kuhusu kupitia Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu kilichofanyika Mkoani Morogoro. Pichani, wa pili kutoka kushoto ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba na wa pili kutoka kulia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.*



*Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Fatma Mwassa (katikati) katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki wa Kikao Kazi cha Wadau cha kutoa maoni kuhusu kupitia Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu kilichofanyika Mkoani Morogoro. Pichani, wa pili kutoka kushoto ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba na wa pili kutoka kulia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.*



# TSC YATAKIWA KUENDELEA KUSHUGHULIKIA KERO NA MALALAMIKO YA WALIMU



*Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Fatma Mwassa (katikati) katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa Sekretarieti iliyoandaa kikao kazi cha wadau cha kupitia rasimu ya andiko la mapitio ya Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu kilichofanyika Mkoani Morogoro. Pichani, wa pili kutoka kushoto ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba na wa pili kutoka kulia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.*



*Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Fatma Mwassa (katikati) katika picha ya pamoja na washiriki wenye taaluma ya ualimu wakati wa kufunga kikao kazi cha kupitia rasimu ya andiko la mapitio ya Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu. Pichani, wa pili kutoka kushoto ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba na wa pili kutoka kulia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.*



*Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba akimpokea Mkuu wa Moka wa Morogoro, Mhe. Fatma Mwassa (wa kwaza kushoto) wakati Mkuu huyo wa Mkoa alipowasili katika Chuo cha Ualimu Morogoro kwa ajili ya kufunga kikao kazi cha kupitia rasimu ya andiko la mapitio ya Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu.*



*Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Fatma Mwassa (katikati) katika picha ya pamoja na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama na Afisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Mwl. Neema Lemunge mara baada ya kufunga kikao kazi cha kupitia rasimu ya andiko la mapitio ya Sheria na Kanuni zote zinazosimamia Utumishi wa Walimu tarehe 27 Aprili, 2023 katika chuo cha Ualimu Morogoro.*

# SHULE MPYA ZA KATA 234 ZA MRADI WA SEQUIP KUPATA VIFAA VYA MAABARA

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) umeomba kuidhinishiwa Shilingi Bilioni 25.34 kwa ajili ya kununua vifaa vya maabara kwa shule mpya 234 za kata na kuendelea na utekelezaji wa uboreshaji wa Elimu ya Sekondari na shughuli nyengine.

Hayo aliyasemwa Mhe. Anjellah Jasmine Kairuki (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), hivi karibuni Bungeni Jijini Dodoma wakati akiwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2023/24.

Alifafanua kuwa matumizi ya fedha hizo zilizoombwa kuidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni pamoja na kununua vifaa vya maabara na kemikali kwa ajili ya shule mpya 234 za Sekondari za Kata zinazojengwa katika Halmashauri mbalimbali hapa nchini.

Waziri Kairuki aliongezea kwa kusema kuwa fedha hizo pia zimepangwa kununua vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya shule 1,000 za Sekondari za Kata kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji, kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi katika maeneo ya ujenzi wa shule mpya za sekondari, kuwezesha utendaji kazi wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI katika utekelezaji wa mradi wa kuboresha Elimu ya Sekondari.

Pia, alisema zitawezesha utangazaji wa shughuli zinazotekelezwa na Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) kwa wananchi ili waweze kufahamu jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuboresha Elimu ya Sekondari nchini na kuwezesha kuwajengea uwezo Watumishi 68 wa Idara ya Usimamizi wa Elimu katika masuala yanayohusu ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP).

Aidha, Mheshimiwa Kairuki baada ya kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 aliliomba Bunge kuridhia kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Trilioni 9.1 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais – TAMISEMI.



# TATUENI CHANGAMOTO ZA WALIMU KULETA MABADILIKO – DKT. MSONDE

**Na. Mwandishi Wetu – Mwanza.**

Maafisa Elimu wa Mikoa na Halmashauri nchini wametakiwa kuwasimamia Walimu kwa weledi na busara katika kutatua changamoto zinazowakabili ili kuleta mabadiliko chanya na yenye tija katika Sekta ya Elimu nchini.

Kauli hiyo ya Serikali ilitolewa Aprili 4, 2023 Jijini Mwanza na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI (ELIMU), Dkt. Charles Msonde, wakati akitoa maelekezo ya Serikali kwa Viongozi hao kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Maafisa Elimu wa Mikoa na Halmashauri Tanzania Bara (REDEOA).

Dkt. Msonde alisema njia pekee ya kuleta mabadiliko kwenye Sekta ya Elimu ni uwajibikaji wa pamoja wa Viongozi katika kuwasaidia Walimu kukabiliana na changamoto zinazowakabili kwenye mazingira yao ya kazi kama vile kuwa na Kanuni ya Ulipaji wa Madeni ya Walimu na kuyakabili masuala yote yanayohusiana na rushwa sehemu ya kazi.

"Itakuwa ni kazi ngumu sana kwa Walimu kuhubiri mabadiliko kama Walimu hawahawa hatutawajali. Changamoto za Walimu ni nyingi na mazingira yao ya utendaji kazi yanahitaji sisi tuwasaidie zaidi." Alisema Dkt. Msonde.

Alisema kuwasimamia Walimu katika ufundishaji unaozingatia watoto kupata ujuzi ambao utaleta matokeo makubwa kuliko ufundishaji wa kuzingatia kumaliza mada kwa wakati bila kuzingatia malengo ya Mkakati wa Ufundishaji na vigezo vyake 22 kama Kusoma, Kuandika na Kuhesabu na umahiri katika somo la kiingereza kwa wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari.

Dkt. Msonde aliwapongeza Viongozi hao kwa kuongeza kiwango cha uwajibikaji wa Walimu nchini kutoka asilimia 30 iliyokuwepo hapo awali mpaka asilimia 60 iliyopo hivi sasa.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Elimu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mwl. Vicent Kayombo, alisema kwa hivi sasa Viongozi hao wanafuatilia kwa karibu ufundishaji wa Walimu shuleni lakini pia ili kuboresha Ufuatiliaji na Usimamizi wa Elimu tayari magari yaliyoagizwa kwa ajili ya Seksheni ya Elimu ya Sekondari yameshawasili na yatapelekwa kwenye maeneo husika.

Kauli Mbiu ya Mkutano huo kwa mwaka 2023 wa REDEOA inasema 'Uboreshaji wa Miundombinu ya Elimu Unaimarisha Ufundishaji, Ujifunzaji na Ustawi wa Walimu na Wanafunzi.'



# TET YASISITIZA WALIMU KUTUMIA VITABU VILIVYO NA ITHIBATI

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.**



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dkt. Aneth Komba, amewataka Walimu kuhakikisha wanatumia vitabu vya kiada na ziada vyenye ithibati ya Kamishna wa Elimu.

Aliyasema hayo hivi karibuni Jijini Dodoma wakati akifungua Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini ya Elimu ya Awali (Watoto Wetu Tunu Yetu) kwa Walimu na Viongozi wa Elimu yanayotolewa na Shirika la "Children in Crossfire."

"Walimu ni chachu ya mabadiliko katika Elimu hivyo nawasisitiza matumizi ya vitabu vya kiada na ziada vilivyo na ithibati ya Kamishna wa Elimu. Ni muhimu sana kutumia vitabu hivi kwani kuna vitabu vingi huko mtaani vyenye maudhui ambayo hayaendani na tamaduni zetu. Nasisitiza kila shule itumie vitabu vyenye ithibati katika kufundisha na kujifunza." Alisema Dkt. Aneth

Aidha, aliwaelekeza Walimu hao kutumia Maktaba Mtandao ya TET ambayo ina vitabu vyote vya kiada na ziada, miongozo, mihtasari na mitaala. Alieleza kuwa maktaba hiyo kwa sasa inapatikana bure kwa mtumiaji mwenye laini ya simu ya Airtel na wapo katika mchakato wa kuongea na kampuni nyingine za simu ziweze kutoa huduma hiyo bure.

Awali, alilishukuru Shirika la Children in Crossfire kupitia mradi wa "Watoto Wetu Tunu Yetu" kwa kuendelea kuwa wadau muhimu katika elimu hususani elimu ya awali katika kuboresha mazingira ya ujifunzaji.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Shirika la "Children in Crossfire" Ndg. Heri Ayubu, alisema kuwa mradi huo wa "Watoto Wetu Tunu Yetu" unatekelezwa katika mikoa mitatu (Mwanza, Morogoro na Dodoma), ukiwa na lengo la kuendelea kuchangia uboreshaji wa utoaji wa Elimu ya Awali nchini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Serikali.

Alisema kuwa, mwisho wa mradi huo wanatarajia kuona ongezeko kubwa la wanafunzi wenye utayari wa kuingia Darasa la Kwanza kwani mafunzo hayo yanawashirikisha Walimu wa Darasa la Awali, Maafisa Elimu, Wadhibiti Ubora na Maafisa Taaluma kutoka Wilaya za Mpwapwa, Bahi na Dodoma Jiji.

# VIONGOZI WA ELIMU WATAKIWA KUONDOA URASIMU NA VIZUIZI VINAVYOKWAMISHA ELIMU

**Na. Mwandishi Wetu – Mwanza.**

Serikali imewaagiza Maafisa Elimu wa Mikoa na Halmashauri nchini kuongeza nguvu ya kusimamia elimu, umahiri, ujuzi na maarifa wanayoyapata watoto ili kuendelea na masomo yao pasipo vizuizi.

Naibu Katibu Mkuu (ELIMU), Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Dkt. Charles Msonde, aliyasema hayo hivi karibuni wakati akifungua Mkutano Mkuu wa Mwaka, 2023 wa Umoja wa Maafisa Elimu wa Mikoa na Halmashauri Tanzania Bara (REDEOA) Jijini Mwanza.

“Katika changamoto ambazo zinawakabili watoto wetu kule shuleni ni ubakaji, ulawiti, usagaji na vitu vingine. Sisi Walimu na sisi Viongozi wengine wote wa Walimu na Walimu wenyewe wote nchini tuna dhamana ya kuliweka na kulitengeneza Taifa letu kwa kuwasimamisha watoto hawa wawe na maadili, uzalendo na utu wema.” Alisema Dkt. Msonde

Naibu Katibu Mkuu huyo alisema pamoja na kuwepo kwa mafanikio ya ufuatiliaji wa elimu nchini bado zipo changamoto kadhaa ambazo viongozi hao wanapaswa kuzishughulikia kwa hali na mali ikiwa ni pamoja na kufuatilia ufundishaji sio tu eneo la Shule bali na Ufundishaji lakini pia namna mtoto anavyopata umahiri na kumudu masomo yake pamoja na wao wenyewe kuacha kufuatilia kwa mazoea kwani wamepewa dhamana ya kuhakikisha Elimu Bora inatokea katika Taifa la Watanzania.

“Bado kabisa ipo changamoto ya ufuatiliaji dhaifu miongoni mwetu sisi. Watanzania wametupa dhamana kufanya kazi hii ya kufanya ufuatiliaji makini na kuhakikisha Walimu wetu wanafundisha kwa weledi na ufasaha mkubwa na umahiri wa watoto wetu unapatikana.” Alisema Dkt. Msonde

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mwl. Vicent Kayombo, alisema katika mkutano wao huo viongozi hao wamekubaliana kuwa baada ya kikao kazi hicho watakwenda kuongea na Walimu shuleni, ikiwa ni matarajio ya kwenda kufanya mapinduzi makubwa ya ufuatiliaji wa ufundishaji wa Walimu darasani lakini pia kuendeleza ushirikiano wa kisekta kati ya Maafisa Elimu Msingi na Sekondari, Wathibiti Ubora, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na wengineo ili kuwa na uelewa wa pamoja na kufanya kazi kama timu.

Kikao Kazi hicho cha Mwaka cha siku tatu kiliambatana na utoaji Tuzo za Viongozi waliofanya vizuri na Wadau waliofanikisha mkutano huo lengo lake likiwa ni kufanya tathmini ya kina na kuja na mbinu mbadala katika kutatua changamoto za elimu nchini.






**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz** **Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania